

MAGEUZI MAKUBWA



Muonekano wa jengo jipya la utawala la Chuo Kikuu Mzumbe.

chuo

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dk Samia Suluhu Hassan, Chuo Kikuu Mzumbe kimefanikiwa kuongeza ajira kutoka watumishi 615 mwaka 2021 hadi 840 mwaka 2025 kati yao wahadhiri ni 432 na waendeshaji ni 408 na hivyo kupelekea kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi iliyokuwa ikikikabili Chuo kwa muda mrefu. Aidha watumishi takribani 347 wameweza kupanda madaraja tangu mwaka 2021.

Kadhalika Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imeweza kulipa Sh 721 milioni ikiwa ni malimbikizo ya madeni ya watumishi waliyokuwa wakiidai Serikali kwa muda mrefu.

**Uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kujifunzia kwa fedha za ndani**

**Ujenzi wa mabweni ya wanafunzi kampasi kuu na Ndaki ya Mbeya**

Chuo Kikuu Mzumbe kwa kutambua uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali chini ya uongozi mahiri wa Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan katika kutatua changamoto za ubora wa miundombinu ya elimu, chuo kiliamua kuunga mkono juhudi za Serikali. Kupitia mapato ya ndani chuo kimefanikiwa kuongeza miundombinu muhimu, ikiwemo ujenzi wa hosteli 4 kampasi kuu, zilizokamilika mwaka 2023 kwa gharama ya Sh 6.7 bilioni.

Majengo haya mapya yameweza kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya malazi.Wanafunzi zaidi ya 1, 0026 wameweza kupata nafasi za malazi na hivyo kuboresha hali ya maisha na masomo kwa wanafunzi.

Aidha Chuo kimeanzisha mradi kujenga hosteli ya wanafunzi wa kike katika Ndaki ya Mbeya ambayo inakabiliwa na changamoto kubwa ya malazi. .

Changamoto hiyo iliifanya Menejimenti ya Chuo kubuni mradi wa ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 800 mradi ambao unatarajiwa kugharimu Sh 5.8 bilioni. Hadi sasa jumla ya Sh 90.2 milioni zimeshakusanywa. Serikali kupitia Wizara ya elimu imeona umuhimu wa kuunga mkono mradi huu, na Chuo kinatarajia kupatiwa fedha toka serikalini ili kuongeza nguvu katika kutelekeza mradi huo.

**Ujenzi wa jengo la utawala na uboreshaji wa barabara za ndani**

Chuo kinakamilisha ujenzi wa Jengo la Utawala katika Kampasi Kuu, mradi wenye thamani ya Sh 4.8 bilioni ambao umelenga kuboresha mazingira ya kazi na huduma kwa wanafunzi, hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji na kuboresha ubora wa elimu inayotolewa. Ujenzi wa jengo hili umefikia asilimia 94 na kukamilika kwake kutaongeza tija kwa watumishi wa chuo.

Kadhalika Chuo kimeendelea kuboresha miundombinu ya barabara za ndani ya Chuo kampasi kuu kwa kujenga barabara za kiwango cha zege zenye urefu wa mita 1,510 pamoja na kufanya

## Sh 50 bilioni

**Fedha ambazo Chuo Kikuu Mzumbe ilipatiwa ikiwa ni bajeti ya utekelezaji wa mradi wa HEET.**

marekebisho katika maeneo ya lami yaliyoharibika. Mradi huu umefikia asilimia 90 ya utekelezaji na utagharimu Sh 924 milioni hadi kukamilika kwake.

**Ujenzi wa zahanati kampasi ya Mbeya na uboreshaji wa kituo cha afya kampasi kuu**

Ili kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na uhakika wa afya zao wakati wote wanapoendelea na masomo, chuo kimeendelea kuimarisha huduma za afya ikiwemo ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati katika Ndaki ya Mbeya ambao umegharimu jumla ya Sh 465.7 milioni na sasa zahanati hii inatoa huduma za afya kwa wanajumuiya ya chuo Kikuu Mzumbe na jamii inayozunguka chuo.

Aidha, Chuo kinakamilisha ujenzi wa jengo la upasuaji katika kituo cha Afya cha Kampasi kuu kwa thamani ya Sh 133.05 milioni ambao kwa sasa umefikia asilimia 90. Hivyo, wanafunzi watanufaika moja kwa moja na huduma bora na za haraka za afya ndani ya Chuo na hatua hiyo itawapa nafasi ya kujikita zaidi kwenye masomo yao na kuboresha ustawi wao wa kitaaluma wawapo chuoni.

**Kuanzishwa kwa kituo cha Tegeta kwa masomo ya shahada za awali Ndaki ya Dar es Salaam**

Chuo Kikuu Mzumbe kimefanikiwa kupanua Ndaki yake ya Dar es Salaam ambayo hapo awali ilikuwa ikitoa masomo ya uzamili pekee katika eneo la Upanga. Mwaka 2021 kwa mara ya kwanza Chuo Kikuu Mzumbe kilianzisha kituo kipya cha Tegeta kwa ajili ya masomo ya Shahada za awali ambapo jumla ya wanafunzi 155 walidahiliwa katika mwaka huo, ambapo wanafunzi 126 walifanikiwa kuhitimu masomo yao katika mahafali ya 22 ya mwaka 2023.

Hadi sasa kituo cha Tegeta kina jumla ya Wanafunzi 758 na kinaendelea kutoa huduma ya masomo kwa kozi za Shahada ya Uhasibu na Fedha-Sekta ya Biashara (Bachelor of Accounting and Finance Business Sector-BAF – BS) na Shahada ya Utawala wa Umma (Bachelor of Public Administration (BPA).

**Kuongezeka kwa miradi ya utafiti na machapisho ya kitaaluma**

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Dk Samia, Chuo Kikuu Mzumbe kimefanikiwa kuandika na kushinda miradi ya tafiti ambayo imelenga kutatua changamoto mbalimbali nchini na kuhudumia jamii. Chuo kimeshiriki kwenye tafiti za maendeleo ya jamii, mazingira, utawala, afya, uchumi, teknolojia, sheria, uhasibu na menejimenti.

Miradi yote hiyo ya tafiti imeweza kuliingizia taifa takribani kiasi cha Dola za Marekani milioni 8.6. Aidha Chuo kimeweza kuonekana kwenye majukwaa ya kitaaluma ya kimataifa kutokana na machapisho mbalimbali yaliyochapishwa na wanataaluma wake.

Zaidi ya machapisho 383 yametolewa kwenye majarida mbalimbali yakiwemo ya ndaniya nchi na ya kimataifa kama vile Scientific Reports (Nature), PloS, Health Science Reports, Scientific African, Women Studies International Forum (Elsevier Science).

**Chuo Kikuu Mzumbe kinavyojivunia uongozi wa Dk Samia Suluhu Hassan**

Chuo Kikuu Mzumbe kinafahamika zaidi kwa ubobezi wake wa kuzalisha viongozi wenye uwezo wa kushughulikia changamoto za kijamii. Rais Dk Samia akiwa ni zao la Chuo Kikuu Mzumbe, ameonyesha uongozi wa kipekee unaozingatia ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi ya maendeleo.

Maamuzi yake yanayozingatia ushahidi yanaendana na msingi wa taaluma ya Chuo Kikuu Mzumbe, ambayo inahimiza matumizi ya utafiti na uchambuzi wa kina katika maamuzi ya kiutawala na kijamii. Kupitia falsafa yake ya 4R, Rais Samia ameonyesha mfano bora wa kutumia maarifa na utafiti katika kukuza utulivu na maendeleo ya kitaifa.

## Sh 32.13 bilioni

**Fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ambazo Chuo Kikuu Mzumbe imezipokea katika kipindi cha miaka minne.**

Rais Samia ameleta mageuzi makubwa katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi, akisisitiza utawala bora na uwajibikaji, mambo ambayo Chuo Kikuu Mzumbe kinayahimiza kwa wahitimu wake. Novemba 24, 2024 Chuo Kikuu Mzumbe kilimtunuku Rais Dk Samia Suluhu Hassan Shahada ya Udaktari wa Heshima katika Uongozi. Maamuzi ya kumtunuku Mheshimiwa Rais heshima hiyo yalizingatia kuwa Chuo kimejikita katika kukuza uongozi bora, uvumbuzi, na maadili katika utumishi wa umma, maadili ambayo Rais Samia ameyaonyesha kwa dhahiri kupitia safari yake ya uongozi na mchango wake kwa taifa.

Katika hotuba yake ya kupokea shahada hiyo, Mhe. Rais alionesha kufurahishwa na kazi inayofanywa na Chuo Kikuu Mzumbe, hususan kubuni na kutelekeza miradi kadhaa ya miundombinu kwa kutumia fedha za ndani na kuahidi ushirikiano toka serikalini kwa kuanzia na mradi wa hosteli ya wasichana Ndaki ya Mbeya.

Maendeleo makubwa ya Chuo Kikuu Mzumbe yaliyopatikana ndani ya muda mfupi kwenye kipindi ambacho Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa madarakani ni uthibitisho tosha wa kazi kubwa inayofanywa na Rais wetu. Uongozi wake mahiri umeleta heshima kubwa kwa nchi yetu katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Maziwa Makuu, Afrika na duniani kote. Hii imejidhirisha zaidi kwenye Diplomasia ya Uchumi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa wawekezaji katika Sekta mbalimbali nchini kwetu.

Tunampongeza sana Mheshimiwa Dk Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka minne akiwa madarakani kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo ameonesha umahiri wa hali ya juu katika kuongoza Watanzania na kusimamia rasilimali za nchi yetu kwa manufaa ya wananchi wote.

Tunamwombea mafanikio makubwa katika kuliongoza Taifa letu ili kuleta maendeleo na mageuzi makubwa ya kijamii na kiuchumi. Sisi wana Jumuiya ya Chuo Kikuu Mzumbe tutaendelea kumuunga mkono kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii zaidi ili kuliletea taifa letu maendeleo pamoja na kuhudumia wananchi tukisimamia kauli mbiu yetu ya Chuo inayosema

*"Tujifunze kwa Maendeleo ya Watu".*



Maendeleo ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe (Kampasi ya Tanga) ambayo ujenzi wake unatekelezwa kupitia fedha za mradi wa HEET.



Maendeleo ya ujenzi wa jengo la taaluma la Chuo Kikuu Mzumbe (Kampasi Kuu) ambalo ujenzi wake unatekelezwa kupitia fedha za mradi wa HEET.